ISSN 2820-2686 | Toleo Na. 4 | Aprili - Juni 2022

# JARIDA LA WAKILI MKUU






## MAKAO MAKUU YA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI YAANZA KUJENGWA MTUMBA, DODOMA

osgtanzania osg_tanzania WAKILI MKUU TV Email: info@osg.go.tz www.osg.go.tz

# BODI YA UHARIRI

## Mwenyekiti

**Dkt. Boniphace Nalija Luhende**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

## Mhariri Mkuu

**Prisca Jackson Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Waandishi wa Jarida

**Sarah Obby Mwakyusa**
Afisa Habari Mwandamizi

**Dennis Julius Buyekwa**
Afisa Habari

## Msanifu wa Jarida

**Nyamhoni Robert Chacha**
Afisa TEHAMA

## Wajumbe

**George Nathaniel Mandepo**
Mkurugenzi wa Usuluhishi

**Abubakar Amin Mrisha**
Mkurugenzi Msaidizi - Usimamizi wa Mashauri

**Kiuye Mbwana Shemakame**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti

**CPA Devota Mathew Ngulugulu**
Mhasibu Mkuu

**Mercy Rowland Kyamba**
Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

**Zuhura Mohamed Kussaga**
Mchumi

# Tahariri ya Mhariri



## Prisca Jackson Ulomi

### Mhariri Mkuu

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imepewa jukumu la uratibu, usimamizi, ushauri na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na Taasisi zake. Katika kutekeleza jukumu hili muhimu, Ofisi inapaswa kushirikiana na taasisi zote za Serikali au taasisi zinazounda mihimili yote mitatu yaani Serikali, Bunge na Mahakama ili kuhakikisha maslahi ya wananchi na nchi kwa ujumla ndani na nje ya nchi yanalindwa ipasavyo.

Katika kutimiza jukumu hilo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliandaa mafunzo ya siku 4 kwa Mawakili wa Serikali zaidi ya 600 kutoka taasisi, idara na Wizara mbalimbali kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali katika kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi kwa ufanisi na kwa kuzingatia maadili stahiki.

Mafunzo haya muhimu yatasaidia Mawakili kutoka taasisi za Serikali kuwa na uelewa wa pamoja kwenye masuala ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano, maridhiano na usuluhishi, utaratibu huo utatoa suluhisho la kuhakikisha migogoro itakayotokea inashughulikiwa kwa haraka na kwa gharama nafuu na kulinda mahusiano mazuri kati ya jamii na Serikali.

## Hongera Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Jarida la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali linatoa pongezi kwa Menejimenti na watumishi wote wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa mafunzo haya ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia filamu ya "*The Royal Tour*" ambayo imetangaza fursa za Tanzania na vivutio vilivyomo ili kuwahabarisha wawekezaji kuja kuwekeza Tanzania.

Kufuatia ujio wa wawekezaji hao, Serikali itaingia mikataba mbalimbali ambayo itahitaji kupata ushauri na majadiliano wakati wa kuingia na pale tofauti zinapokuwa zimejitokeza kati ya Serikali na wawekezaji, Mawakili wa Serikali watahusika kuiwakilisha Serikali katika migogoro husika, hivyo, mafunzo haya ni muhimu kwa kila mmoja na yamefanyika wakati muafaka.

Baada ya mafunzo haya ni mategemeo yetu kuwa idadi ya mashauri ya madai na usuluhishi yanayofunguliwa na yanayoendelea yatapungua kwa kuyamaliza kwa njia ya majadiliano, maridhiano na usuluhishi hivyo kuimarisha juhudi za Serikali katika kuvutia wawekezaji na kutekeleza miradi mbalimbali nchini.

Aidha, tunatarajia kuona mafunzo haya yanakuwa chachu katika utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano, maridhiano na usuluhishi kutokana na elimu na stadi za utatuzi wa migogoro Mawakili walizopata kutoka kwenye mafunzo haya na kuiwakilisha vyema Serikali na taasisi kwenye mashauri yake ndani na nje ya nchi.

Ni matumaini yetu Mawakili wa Serikali wataendelea kuishauri vizuri Serikali na taasisi zake kuhusu namna bora ya kumaliza migogoro na wananchi au wawekezaji bila kuathiri maslahi ya nchi.

# Kutoka Kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri



**Dkt. Boniphace N. Luhende**

**Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

### Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Tunashukuru tena kuungana na wasomaji wetu wapendwa kwenye toleo la Nne la Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali. Jarida hili linajumuisha matukio yote muhimu yaliyotokea kwa kipindi cha mwezi Aprili, 2022 hadi mwezi Juni 2022. Katika kipindi hiki, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuhakikisha inaendelea kuiwakilisha vyema Serikali na taasisi zake kwenye mashauri ya madai na usuluhishi.

Sanjari na kutimiza majukumu yake, Ofisi imepata mafanikio mbalimbali kwenye kipindi cha robo ya mwisho (Aprili - Juni) ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Hata hivyo, Jarida limeangazia maeneo makubwa matatu ambayo ni uendeshaji wa mashauri mbalimbali ya Serikali; mafunzo kwa Mawakili wa Serikali; na ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika Mji wa Serikali uliopo eneo la Mtumba, Dodoma.

Kupitia Jarida hili tutajionea wazi jitihada, ushirikiano na umoja uliopo si tu baina ya wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali bali pia baina ya Ofisi hii na Wizara na taasisi nyingine. Tumejionea wazi ushirikiano na umoja ulivyowezesha kufanyika kwa mafunzo ya Mawakili wa Serikali takribani 600 kutoka kwenye Wizara 24 na taasisi 91 za Serikali. Ni rai yetu kuwa umoja huu ukiendelea kwenye kuendesha mashauri ya Serikali utasaidia kulinda mali za umma; kuokoa fedha za walipa kodi; na kuimarisha utawala wa sheria kwenye nchi yetu.

Pia, tunaendelea kutoa shukrani zetu za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupa fedha za kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mji wa Serikali, Mtumba - Dodoma. Kwetu ni hatua kubwa sana, tunashukuru kwa kutuamini na kutupa nafasi ya kuwa na jengo letu la kwanza kama Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Mwisho, niwahimize watanzania washiriki kikamilifu katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi litakalofanyika tarehe 23 Agosti, 2022. Zoezi hili ni muhimu sana katika kupanga mipango ya maendeleo ya nchi. "Sensa Kwa Maendeleo; Jiandae Kuhesabiwa". Nawatakia usomaji mwema.

Asanteni.

# Yaliyomo


06 UJENZI WA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI WAANZA

07 SERIKALI YATAMBUA UMUHIMU WA MAWAKILI

10 MAWAKILI WA SERIKALI WATAKIWA KUZINGATIA MAADILI

12 SERIKALI YAENDESHA MASHAURI KWA NJIA YA MTANDAO

14 WAFANYAKAZI MFAHAMU WAJIBU WENU MAHALA PA KAZI

18 WATUMISHI WATAKIWA KUPIMA AFYA ZAO

20 SERIKALI YAENDESHA MAFUNZO KWA MAWAKILI WAKE

22 MAWAKILI FANYENI UTAFITI KABLA YA MAJADILIANO YA MIGOGORO

24 UENDESHAJI WA USULUHISHI ULIOPO MAHAKAMANI

26 MFUMO WA UTATUZI WA MIGOGORO YA KODI NCHINI TANZANIA

28 USULUHISHI, USIMAMIZI NA UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA MIKATABA YA UJENZI

30 UENDESHAJI WA MASHAURI YA HAKI ZA BINADAMU

32 WATUMISHI WAANDALIWA KUWA VIONGOZI MAHIRI

35 RAIS SAMIA: NITABORESHA MASLAHI YA WAFANYAKAZI NCHINI

37 SERIKALI YAKABIDHIWA MASHAMBA YA TANZANIA PLANTATIONS LTD

39 MAHAKAMA YAAMURU WABUNGE 19 WA CHADEMA KUENDELEA NA UBUNGE

41 BARAZA LAKAMILISHA MKATABA WA KWANZA

42 WATUMISHI WASHIRIKISHWE UONGOZI WA PAMOJA

44 WATUMISHI WATEMBELEA HIFADHI YA TAIFA TARANGIRE




*Picha ya pamoja kati ya wawakilishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) wakiongozwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (aliyesimama mbele katikati) watumishi wa TBA na SUMA JKT baada ya makabidhiano ya eneo la ujenzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mtumba - Dodoma.*

# UJENZI WA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI WAANZA

Wawakilishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) wakiongozwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende tarehe 18 Juni, 2022 walishuhudia makabidhiano ya eneo la ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali lenye ukubwa wa mita za mraba 17,342.

Makabidhiano hayo yamefanyika kwenye Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma baina ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ambaye ni Mshauri Elekezi aliyewakilishwa na Msanifu Majengo Weja Ng'olo na Kampuni ya Ujenzi ya SUMA JKT ambae ni Mkandarasi iliyowakilishwa na Mkadiriaji Majenzi, Jacob Ghati.

Akikabidhi eneo hilo, mwakilishi wa TBA, Ng'olo alieleza kuwa jengo la Ofisi linalotarajiwa kujengwa ni la kisasa na ni miongoni mwa majengo yenye muonekano mzuri katika Mji wa Serikali Mtumba. Jengo hili litakuwa na miundombinu mbalimbali ikiwemo vyumba vya Ofisi 127, maegesho ya magari 111, maktaba, kumbi 2 za mikutano zenye nafasi 108 kila mmoja, kumbi 2 za kutolea mafunzo zenye nafasi 42 kila mmoja, maabara ya kompyuta, vyumba vidogo 10 vya mikutano na chumba kwa ajili ya akina mama wanaonyonyesha watoto wakiwa kazini. Ujenzi wa jengo hilo unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi kumi na nane (18).

Akizungumza kwa niaba ya Mkandarasi, Ghati alisema kuwa wako tayari kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa mujibu wa mkataba na kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi (TBA) na Mshitiri (OWMS).

Kwa upande wake, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Luhende aliwatakia Mkandarasi na Mshauri Elekezi utekelezaji mwema wa majukumu yao kwa mujibu wa mkataba na kwa kuzingatia weledi. Pia aliwahakikishia kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu Serikali itawapa ushirikiano unaostahili.




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Mary Makondo akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) yaliyofanyika jijini Arusha.*

# SERIKALI YATAMBUA UMUHIMU WA MAWAKILI

Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Mary Makondo ameipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa weledi na kushiriki uandaaji wa nyaraka, kusimamia mashauri yaliyofunguliwa na Serikali au dhidi yake katika sekta zote na taasisi za serikali.

Akifungua mafunzo ya Mawakili wa Serikali yaliyoandaliwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Arusha, Bi. Makondo alisema mafunzo hayo ya siku nne yatawajengea uwezo zaidi wa kuisimamia Serikali katika utekelezaji wa miradi mikubwa na ya kimkakati.

"Nawapongeza sana kwa kuisaidia Serikali katika kutekeleza majukumu yake na kuokoa fedha kutoka kwenye mashauri ya madai ambazo zimesaidia kuendelea kutumika katika ukuaji wa uchumi wetu, nyie ni watu muhimu sana kwenye ukuaji wa uchumi na uboreshaji wa pato la Taifa," alisema.

Bi. Makondo alisema Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa kiungo cha mihimili ya dola yaani Serikali, Bunge na Mahakama katika uratibu, usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi yanayofunguliwa dhidi ya au kwa niaba ya mihimili hiyo.

"Tumeona Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imechangia katika uokoaji wa mapato ya Serikali kwa kusimamia ipasavyo katika mashauri yaliyopo ndani na

nje ya nchi katika migogoro inayoibuka katika utekelezaji wa mikataba mbalimbali", alisema Bi. Makondo.

Alisema kuwa Serikali inatambua ya kwamba inawajibu wa kuwapatia Mawakili mafunzo mara kwa mara kadri bajeti itakavyoruhusu ili kuendelea kuwajengea uwezo wa kuandaa nyaraka kwa kuzingatia misingi ambayo ipo kisheria pamoja na kanuni.

Bi. Makondo alifurahishwa na uwezo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika uratibu, usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.

Aidha, aliipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuwa mstari wa mbele kutatua migogoro inayoibuka katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuhakikisha maslahi ya nchi yanalindwa na kuwataka kujiandaa ipasavyo katika kupata elimu na stadi ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya maridhiano, majadiliano na suluhisho inayoibuka kwenye taasisi za Serikali za ndani na nje ya nchi.

"Tumeshuhudia migogoro hii imekuwa ikiongezeka na nyie ni watu muhimu na Serikali inatambua mchango wenu mkubwa na wengine mnahusika kutoa ushahidi, uandaaji wa nyaraka na katika uendeshaji wa mashauri hayo iwapo mtaandaa vizuri nyaraka pamoja na kutoa ushauri itasaidia Serikali kuiepusha na ulipaji wa fidia kwa wadau," alisema Bi. Makondo.

Naye Wakili Mkuu wa Serikali, Mhe. Gabriel Malata alisema mafunzo yatawajengea uwezo Mawakili wa Serikali katika kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi na majadiliano, hivyo kuongeza ufanisi katika taasisi zao na kutokana na maendeleo ya sayansi na



*Baadhi ya Mawakili wa Serikali wakimsikiliza Mgeni Rasmi (hayupo pichani) wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha.*

teknolojia, uchumi, siasa na utamaduni kumekuwa na uhitaji wa mafunzo endelevu ili kuendana na mabadiliko yanayojitokeza katika taaluma ya sheria nchini na duniani kote.

Mhe. Malata alisema pamoja na mambo mengine katika mafunzo, Mawakili wanatarajia kufundishwa masuala ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi na majadiliano, utaratibu unaotoa suluhisho la kuhakikisha migogoro itakayotokea kwenye uwekezaji na ujenzi wa viwanda inashughulikiwa kwa haraka, kwa gharama nafuu na pia utalinda mahusiano ya kibiashara kati ya wawekezaji na Serikali yetu.

Alisema Ofisi inashiriki kikamilifu katika kukuza uchumi ikiwemo kushiriki kwenye utatuzi wa migogoro na mashauri kwa wakati na kwa kushirikiana na vyombo vya utoaji haki, pamoja na kutoa ushauri kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kutatua migogoro mbalimbali kwa njia ya majadiliano.

"Lakini tumeendesha

mashauri ya madai na usuluhishi kwa weledi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake na kuokoa fedha na mali nyingine za Serikali ambazo watu wasiostahili wangeweza kulipwa, mfano tangu kuanzishwa Ofisi hii, tumeokoa zaidi ya shilingi trilioni kumi na fedha hizi zimeendelea kutumika katika utoaji wa huduma na kukuza uchumi wa nchi," alisema Mhe. Malata.

Aidha, Mhe. Malata alisema Ofisi imeona ni vyema kuwa na mafunzo ambayo wakufunzi wake ni Majaji, Majaji wastaafu pamoja na wawezeshaji wengine waliobobea katika masuala mbalimbali kwenye tasnia ya sheria ili waweze kutoa mafunzo haya muhimu kwa Mawakili wa Serikali.

"Tutaendelea kutoa mafunzo ya kisasa ya jumla na maalumu kwa Mawakili wote ili waweze kuiwakilisha ipasavyo Serikali katika nyanja zote zikiwemo za uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi", alisema Mhe. Malata

Mhe. Malata alisema pamoja na kuwa na kipaumbele hicho Ofisi inaendelea kutambua umuhimu wake kwa mihimili yote ya dola, na kipekee kutambua juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita zinazofanywa na Mhe. Samia Hassan Suluhu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuvutia wawekezaji nchini.

"Ofisi inaendelea kushirikiana na taasisi zote za Serikali ambazo zipo kwenye mihimili hii mitatu yaani Serikali yenyewe, Bunge na Mahakama ili kuhakikisha maslahi ya wananchi ndani na nje ya nchi yanalindwa ipasavyo," alisema Mhe. Malata.

Wakili wa Serikali kutoka Wakala wa Vipimo Laurencia Callist aliishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo yanawajenga kiuwezo katika utendaji kazi wao na kuamini kuwa taasisi zao zitakwenda kunufaika na mabadiliko ya utendaji kazi wao baada ya mafunzo.

"Ni nadra sana kwa Mawakili wa Serikali kupata fursa za mafunzo kama haya, niipongeze Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kutupatia nafasi hii na tunaamini tutajifunza mengi na kwenda kubadilika katika kuisimamia Serikali kwenye kuendesha mashauri", alisema Callist.



*Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Mary Makondo (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mawakili wa Serikali wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha. Kushoto kwake ni Wakili Mkuu wa Serikali, Mhe. Gabriel Malata na kulia kwake ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende.*




*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) akizungumza wakati wa kufunga mafunzo kwa Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) yaliyofanyika jijini Arusha.*

# MAWAKILI WA SERIKALI WATAKIWA KUZINGATIA MAADILI

Mawakili wa Serikali nchini wametakiwa kuendelea kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma, nidhamu, uzalendo, uwajibikaji na moyo wa kufanya kazi kwa bidii pamoja na kuendelea kupinga vitendo vya rushwa katika utumishi wa umma

Wito huo ulitolewa na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb.) wakati akifunga mafunzo ya Mawakili wa Serikali jijini Arusha yenye lengo la kuwajengea uwezo mawakili hao katika kusimamia mashauri kwenye taasisi zao

"Maadili yetu yanatuambia tuepuke rushwa kwani itakufikisha pabaya na haina siri, utapokea kwa siri lakini matendo yako yataanza kujionyesha hivyo endeleeni kufanya kazi kwa kuzingatia maadili," alisisitiza Mhe. Dkt. Ndumbaro.

Dkt. Ndumbaro aliwataka Mawakili kuwa na utumishi wenye ufanisi na kuheshimika na wanapaswa kufuata Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma kwa kuwa na tabia na mienendo unaozingatia utoaji wa huduma bora, utii kwa Serikali, utoaji wa huduma bila upendeleo, kufanya kazi kwa uadilifu, kuwajibika kwa umma, kuheshimu sheria za nchi na kuepuka vitendo vyovyote vya ukiukwaji wa mambo tajwa ikiwemo kushawishi na

kupokea rushwa.

Alisema kuwa matarajio ya Serikali ni kuona Mawakili wanakuwa chachu katika utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano, maridhiano na usuluhishi kutokana na elimu na stadi za utatuzi wa migogoro walizonazo kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi

“Natarajia kuona mnapunguza idadi ya mashauri ya madai na usuluhishi yanayofunguliwa na yanayoendelea kwa kuyamaliza kwa njia ya majadiliano, maridhiano na usuluhishi hivyo kuimarisha juhudi za Serikali katika kuvutia wawekezaji na kutekeleza miradi mbalimbali nchini”, alisema Mhe. Dkt. Ndumbaro

Aliongeza kuwa matarajio ya Serikali ni kuona Mawakili hawabweteki kutokana na utendaji mzuri ulioleta mafanikio makubwa tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali bali iwe sifa na chachu ya kuwafanya waendelee kufanya vizuri zaidi.

“Ofisi hii ni moja kati ya Ofisi changa kabisa katika Wizara ya Katiba na Sheria lakini ni taasisi ambayo tangu kuanzishwa kwake imeifanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu, utendaji kazi wa Ofisi hii unaonekana bayana kwa kuokoa fedha nyingi na mali za Serikali kwa hiyo, Ofisi hii ni muhimu sana katika Wizara yetu na Serikali yetu na mnafanya kazi kubwa sana,” alisema Dkt. Ndumbaro

Alieleza kuwa ni lazima wajipange kuhakikisha wanaendelea vizuri na endapo wameelewa mada walizofundishwa vizuri na kwenda kuzitekeleza na kuziishi na kuwataka kwenda kupunguza migogoro ambayo Serikali inaingia.

“Kama Wizara ya Katiba na Sheria tutaendelea kuwapa ushirikiano kila itakapohitajika lakini pia tunatarajia kwamba mafunzo haya yataenda kuwa chachu ya utatuzi wa migogoro mbalimbali ya kisheria ambayo inaikabili Serikali na taasisi zake pamoja na kwenda kupunguza mashauri kwenye Mahakama na maeneo mengine ambayo Serikali inakabiliana nayo,” aliongeza Dkt. Ndumbaro.

Alifafanua kuwa wakifanikiwa kutekeleza ipasavyo na mashauri yakapungua itaokoa gharama ambayo Serikali inatumia lakini muhimu zaidi wataenda kutekeleza kazi yao ya kuishauri Serikali ili isiweze kupata mashauri mbalimbali.

Sambamba na hayo, aliwataka kuwa wa kwanza kuziheshimu sheria pamoja na kupambana na rushwa kwani wako kwenye mfumo wa kutoa haki na rushwa ni adui wa haki hivyo ni lazima waepuke jambo hilo pamoja na kwamba kesi wanazoziendesha ni kubwa na zina majaribu mengi.

Akimkaribisha mgeni rasmi, Wakili Mkuu wa Serikali, Mhe. Gabriel Malata alisema mafunzo haya yamewajengea na yataendelea kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali katika kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi na majadiliano hivyo kuongeza ufanisi katika taasisi zao

“Kwa kutambua hilo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliona umuhimu wa kuandaa mafunzo ambayo yamehudhuriwa na Mawakili wa Serikali kutoka taasisi mbalimbali za Serikali ambapo ni matarajio yetu yamewaongezea ujuzi wa kuweza kutekeleza ipasavyo majukumu yao”, alisema Mhe. Malata

Mhe. Malata alisema kuwa suala la utatuzi wa migogoro katika maendeleo ya nchi yoyote ni jambo lisilo epukika na katika mafunzo haya tumefundishwa masuala ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi na majadiliano, utaratibu unaotoa suluhisho wa kuhakikisha migogoro itakayotokea kwenye uwekezaji inashughulikiwa haraka.

Mhe. Malata alisema kuwa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri yote yanayohusiana na Serikali na taasisi zake yanayofunguliwa ndani na nje ya nchi pamoja na kuingilia kati na kuendesha mashauri yanayohusu Serikali na taasisi zake hasa katika mashirika na kampuni ambazo Serikali inakuwa ni mwanahisa muhimu.

“Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni kiungo kati ya Wizara ya Katiba na Sheria na mihimili yote mitatu ambapo kupitia Mawakili hawa tumeendelea kuhakikisha kwamba tunaendesha na tunapunguza mashauri yote yaliyopo Mahakamani na ambayo hayajafunguliwa ili kuhakikisha kwamba tunapunguza idadi ya migogoro na mashauri,” alisema Mhe. Malata.

# SERIKALI YAENDESHA MASHAURI KWA NJIA YA MTANDAO



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende ( aliyeketi katikati) akiendesha kikao kwa njia ya mtandao katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuendesha mashauri kwa njia ya mtandao (video conference) ikiwa ni hatua mojawapo ya kupunguza gharama za uendeshaji wa mashauri pamoja na kujikinga na maambukizi ya virusi vinavyosababisha ugonjwa wa UVIKO-19.

Uboreshaji wa miundombinu ya TEHAMA katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali umesaidia usikilizwaji wa Mashauri hayo kwa njia ya mtandano hatua iliyowasaidia watumishi wa Ofisi hii kote nchini pamoja na wadau wake kuweza kujikinga dhidi ya maambukizi ya ugonjwa

hatari wa UVIKO-19 ulioanza kusambaa duniani kote tangu mwishoni mwa mwaka 2019.

Maboresho ya miundo mbinu yaliyofanyika yalihusisha ufungaji wa vifaa vya kisasa ikiwemo ununuzi wa runinga kubwa, vifaa vya kuwezesha mtandao kupatikana muda wote sambamba na kuongeza uwezeshaji wa upatikanaji wa miundombinu na mifumo salama na ya kuaminika ya Serikali Mtandao ndani ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Akizungumzia namna ya uendeshaji wa mashauri kwa kutumia teknolojia hiyo, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA, Azizi Makaburi alisema njia hiyo imerahisisha uendeshaji wa mashauri katika mikoa mbalimbali na sasa wanaweza kuendesha mashauri hayo kutoka sehemu yoyote duniani.

"Kabla ya kuanza kutumia teknolojia hii, Ofisi ilitumia gharama kubwa ya kusafirisha watumishi hasa Mawakili kwa lengo la kuendesha mashauri haya, lakini sasa gharama za uendeshaji wa mashauri zitapungua kwa kiasi kikubwa kwa kuwa hawatalazimika kusafiri tena na sasa mashauri mengi yataendeshwa kutokea hapahapa", alisema Makaburi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Madai anayeshughulikia Mashauri ya Katiba, Haki za Binadamu, na Uchaguzi Hangi Chang'a alisema kuwa ujio wa matumizi ya TEHAMA umekuja muda muafaka hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali ya Awamu ya Sita imejidhatiti kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo kwa ufasaha zaidi.

Alisema kuwa matumizi ya Teknolojia hii yameisadia sana Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuendesha mashauri kwa wakati hasa mashauri yaliyopo katika Mahakama ya Afrika Mashariki na ile ya Haki za Binadamu zilizopo Jijini Arusha.

Uwepo wa huduma hii umewasaidia Mawakili kufika Mahakamani kwa wakati, lakini pia umewapa fursa Mawakili kufanya maandalizi ya kutosha hatua ambayo imesaidia kuendesha mashauri hayo kwa ufasaha na kuipatia Serikali ushindi kwenye mashauri mengi yaliyofunguliwa dhidi yake au iliyoyafungua dhidi ya watu na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Naye Wakili Mkuu wa Serikali, Mhe. Gabriel Malata akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake alisema kuwa moja ya mafanikio makubwa ya matumizi ya TEHAMA katika shughuli za usimamizi na uendeshaji wa mashauri ni kuwepo kwa mfumo wa Kielekitroniki wa Kusajili, Kusimamia, Kuendesha na Kuratibu Mashauri (Case Inventory Management System) uliozinduliwa mwishoni mwa mwaka 2019.

Akielezea namna mfumo huo unavyofanya kazi, Mhe. Malata alisema kuwa mfumo huo umeweza kurahisisha usajili wa mashauri Mahakamani; kuwapangia Mawakili mashauri ya kuendesha pamoja; na kutunza kumbukumbu za mashauri kuanzia yanaposajiliwa mpaka hatua ya kutolewa uamuzi.

Aliongeza kuwa uwepo wa mfumo huo umesaidia kurahisisha uendeshaji wa mashauri hayo kwani sasa imekuwa rahisi kufanya ufuatiliaji ambapo sasa tunaweza kujua jalada husika liko kwa Wakili gani na hatua lilipofikia na hivyo kuwa rahisi kuongeza nguvu kwa yale mashauri yanayoonekana kuwa na maslahi mapana kwa lengo la kuipatia ushindi Serikali.



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb) akifungua kikao cha Pili cha Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika jijini Dodoma.*

# WAFANYAKAZI MFAHAMU WAJIBU WENU MAHALA PA KAZI

> "Kila mtumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ahakikishe anafahamu wajibu wake mahala pa kazi ili aweze kutekeleza malengo aliyopangiwa na kuhakikisha anayakamilisha katika muda uliopangwa," alisisitiza Mhe. Pinda (Mb).

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb), alisema ni wajibu wa kila mtumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) kuhakikisha anafahamu wajibu wake mahala pa kazi ili aweze kutekeleza malengo aliyopangiwa na kuhakikisha anayakamilisha katika muda uliopangwa hatua itakayosaidia Ofisi hiyo kufikia malengo yake kwa wakati.

Aliyasema hayo wakati akifungua Kikao cha Pili cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 kilichofanyika jijini Dodoma wakati wa kupitia makisio ya bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/23.

Akizungumzia bajeti ya OWMS, Naibu Waziri Pinda alisema anaamini Ofisi hiyo itakuwa imeandaa bajeti yake kwa kufuata utaratibu wa Mpango wa Matumizi ya Muda wa Kati (Medium Term Expenditure Framework) kwa kuwa huu ndio utaratibu ambao bajeti huandaliwa kulingana na mipango iliyoainishwa kwenye mpango kazi wa taasisi husika kwa kuzingatia vyanzo vya mapato na rasilimali zilizopo kwa sababu mtindo huu wa bajeti unaonesha wazi utendaji wa kila idara hususani kwa mtu mmoja mmoja kulingana na vipimo vya utendaji kazi wake.

“Nichukue nafasi hii kuwataka wafanyakazi wa OWMS kufuata utaratibu unaoelekezwa na bajeti husika. Mtakapokuwa mnafanya mapitio ya bajeti ya nusu mwaka hapo baadaye, mtaona ni nani au Idara gani haikufanya kazi kulingana na malengo ya OWMS na hivyo kupata nafasi ya kurekebisha mapungufu mtakayoyabaini,” alisema Mhe. Pinda.

Aidha, Mhe. Pinda aliwahakikishia wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Wizara kuwa wataendelea kuiunga mkono Ofisi hiyo kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya huku wakiendelea kufanyia kazi changamoto ambazo zimekuwa zikiwakabili ili waweze kuongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

> **Kwa kushirikiana na Wizara tutaendelea kuiunga mkono Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri mnayoendelea kuifanya na tutaendelea kufanyia kazi changamoto ambazo zimekuwa zikiwakabili ili muweze kuongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yenu ya kila siku.**

Kuhusu namna atakavyoshughulikia changamoto nyingine, Waziri Pinda aliahidi kuzichukua na kuzishughulikia kwa kushirikiana na viongozi wengine wa Serikali ikiwa ni pamoja na kuziwasilisha zile changamoto za kiutumishi kwa Wizara husika ili ziweze kushughulikiwa kwa mujibu wa kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Akitoa wito kwa wajumbe wa Baraza la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mhe. Pinda aliwataka wajumbe hao kulitumia Baraza la Wafanyakazi kuhimiza kila mtumishi kujua wajibu wake wa kutumia muda wa kazi ipasavyo kwa kufanya kazi kwa bidii ili kuiwezesha OWMS kusonga mbele katika kutekeleza maagizo ya Serikali pamoja na kutoa huduma stahiki na kwa wakati.

Awali Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Nalija Luhende, Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, alisema kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliongezewa bajeti yake kutoka shilingi bilioni 11.48 kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi bilioni 12.13 kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 5.4.

Dkt. Luhende alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa Ofisi yake uliopelekea kuongezeka kwa bajeti hatua ambayo itasaidia Ofisi kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha pamoja na kupunguza changamoto za ufinyu wa bajeti zilizokuwepo awali.

Kuhusu mashauri yaliyoendeshwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Makamu Mwenyekiti wa Baraza hilo, Dkt. Luhende alisema kuwa Ofisi hiyo imefanikiwa kuendesha mashauri ya madai 1,102 na ya usuluhishi 117 na hivyo kufanya jumla ya mashauri yaliyoendeshwa kwa kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Serikali ya awamu ya sita kuwa 1,219.

Dkt. Luhende aliongeza kuwa jumla ya mashauri 450 yalimalizika ambapo mashauri ya madai yaliyomalizika na Serikali kushinda ni 444 huku mashauri ya usuluhishi yakiwa 6 na kupelekea Serikali kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 236.6 ambazo kama Serikali ingeshindwa basi kiasi hicho cha fedha kingelipwa kwa walalamikaji waliofungua mashauri hayo katika Mahakama mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Aidha, akizungumzia eneo la rasilimali watu, Dkt. Luhende alisema kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imeweza kujaza nafasi mbalimbali za ajira ambazo zimesaidia kujaza nafasi zilizokuwa wazi kwa lengo la kuongeza nguvu katika maeneo ya kada mbali mbali ndani ya Ofisi hiyo.

"Tumefanikiwa kupata vibali vya kuajiri watumishi 23 wapya, watumishi 3 kwa nafasi ya ajira mbadala na mtumishi 1 wa kuhamia. Aidha, Ofisi iliweza kujaza nafasi hizo na kufikia jumla ya watumishi 159," alisema Dkt. Luhende.



*Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiimba wimbo wa Mshikamano Daima wakati wa ufunguzi wa kikao cha Baraza hilo kilichofanyika jijini Dodoma.*




*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb.) (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kufungua kikao cha Baraza hilo kilichofanyika jijini Dodoma.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija Luhende akimkaribisha Mgeni Rasmi Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (aliyeketi katikati) kufungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo kilichofanyika jijini Dodoma.*



*Afisa Tawala, Mariam Bundala (kulia) akifanya kipimo wakati wa zoezi la kupima afya kwa hiari lililofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Dar es Salaam.*

# WATUMISHI WATAKIWA KUPIMA AFYA ZAO

Wito umetolewa kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kupima afya zao mara kwa mara ili kutambua afya zao kama ambavyo mwongozo wa kudhibiti virusi vya (VVU) UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukiza mahala pa kazi unavyowataka.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu James Kibamba kwenye mafunzo pamoja na upimaji afya kwa watumishi wa umma yaliyosimamiwa na wataalamu kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam yaliyofanyika kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Dar es Salaam.

Kibamba alisema kuwa zoezi la upimaji wa afya ni muhimu kwa watumishi waliopo kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutokana na watumishi kukosa muda wa kuchunguza afya zao katika vituo vya kutolea huduma za afya.

"Tumesogeza huduma karibu kutokana na majukumu mengi waliyonayo watumishi na kukosa muda wa kuchunguza afya zetu. Kupima afya ni jambo la lazima na muhimu sana kwa mtumishi kwani itasaidia hata kuongeza tija katika taasisi baada ya kutambua afya yake" alisema Kibamba.

Aidha, alisema kuwa kwa kutambua afya za wafanyakazi kutamwezesha mwajiri kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Ofisi na kuwataka watumishi hao kutumia fursa iliyopo kuchunguza afya zao.

"Kama mtumishi atakuwa na afya njema basi atasaidia kuongeza uzalishaji katika taasisi hivyo wafanyakazi wanatakiwa kupima afya zao kwa mujibu wa mwongozo huo wa kudhibiti VVU, UKIMWI, pamoja na magonjwa sugu yasiyoambukiza" alisisitiza Kibamba.

Mratibu wa zoezi hilo Geofrey Annania alisema kuwa watumishi wanatakiwa kupima afya zao na kujua

namna wanavyoweza kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza kwani limekuwa janga kwa jamii kwa sababu ya kukosa muda wa kufanya mazoezi na kuangalia afya zao.

"Muda mwingi watumishi wetu wanautumia ofisini na Mahakamani wanakosa fursa za kuangalia afya zao hivyo kuonyesha wengi wana tatizo la uzito kupindukia pamoja na msongo wa mawazo, kwa hiyo mafunzo haya yatawasaidia kutambua wafanye nini ili kuepuka kupata magonjwa hayo sugu yasiyoambukiza," alisema Annaniah.

Alisema kuwa kupitia mafunzo hayo wafanyakazi, watapatiwa mada mbalimbali kutoka kwa watalaam wa masula ya afya.

"Wafanyakazi wanatakiwa pia kufanya mazoezi ili kuondokana na tatizo la uzito uliopitiliza pamoja na msongo wa mawazo", alisema Annaniah.

Alisema lengo la utoaji wa huduma hizi ni kusogeza huduma za afya kwa watumishi ili kupata elimu, ushauri, uchunguzi na huduma za afya sehemu za kazi kwa wakati. Mafunzo ya huduma ya afya ya mkoba yaliandaliwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mganga Mkuu wa Ofisi ya Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam kupitia idara ya Afya.

Kwa upande wake mtoa mada katika mafunzo hayo Mratibu wa Magonjwa Yasiyoambukiza Dkt. Milka Mathania kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam alisema lengo la mafunzo hayo ni kuongea na watumishi ili kuwasaidia kujenga tabia ya kupima afya zao mara kwa mara na sio kusubiri mpaka ugonjwa uwapate.

Dkt. Mathania alisema mafunzo haya yalikuwa na lengo la kutoa huduma na fursa kwa wafanyakazi kupima afya zao na mwenendo wa magonjwa yasioambukiza pamoja na kukinga na kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO 19.

Alisema kuwa jumla ya watumishi 79 walipata mafunzo na huduma ya afya kwa kupima uzito (BMI), kupima kiwango cha sukari (RBG), kupima maambukizi ya Virusi vya UKIMWI pamoja na kupata ushauri nasaha na chanjo ya UVIKO19.



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Nalija Luhende (kulia), akipata elimu ya afya na upimaji wa magonjwa yasiyoambukiza, VVU/UKIMWI na utoaji chanjo ya UVIKO 19 kutoka kwa mtaalamu wa Afya kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri yaJiji la Dar es Salaam.*




*Dkt. Ringo Tenga, Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam akitoa mada ya Sheria ya mikopo ya nyumba (rehani) katika mafunzo ya Mawakili wa Serikali jijini Arusha.*

# SERIKALI YAENDESHA MAFUNZO KWA MAWAKILI WAKE

> "Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inapaswa kuwa mstari wa mbele katika kulinda maslahi ya nchi."
>
> Bi. Mary Makondo**, Katibu Mkuu.**

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliandaa mafunzo ya kimkakati kwa lengo la kuwajengea ujuzi na uwezo Mawakili ili kuboresha utekelezaji wa majukumu kwa Mawakili wa Serikali kwa ufanisi mkubwa na kuwezesha Serikali kupata matokeo chanya katika taasisi zake.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo alifungua mafunzo hayo ya siku nne ambayo yalihusisha Mawakili wa Serikali kutoka taasisi za Serikali 92 na Wizara 24.

Akimkaribisha mgeni rasmi, Wakili Mkuu wa Serikali Mhe. Gabriel Malata alisema mafunzo yatawajengea uwezo Mawakili wa Serikali katika kusimamia mashauri ya Serikali na utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi na majadiliano hivyo kuongeza ufanisi katika taasisi zao.

Mhe. Malata alisema pamoja na mambo mengine katika mafunzo hayo Mawakili walifundishwa masuala ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi na majadiliano, utaratibu unaotoa suluhisho la kuhakikisha migogoro itakayotokea kwenye uwekezaji na ujenzi wa viwanda inashughulikiwa kwa haraka, kwa gharama nafuu na pia kutalinda mahusiano ya kibiashara kati ya wawekezaji na Serikali yetu.

Akifungua mafunzo hayo, Bi. Makondo aliipongeza OWMS kwa kushirikisha mihimili yote katika mafunzo hayo na kwa kupitia sera ya nchi Serikali inafanya juhudi mbalimbali kuhakikisha kuwa wawekezaji wanavutiwa na kuwekeza nchini, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inapaswa kuwa mstari wa mbele katika kulinda maslahi ya nchi.

Aidha, mada mbalimbali zilizowasilishwa kwa Mawakili ni pamoja na taratibu za usuluhishi; usuluhishi ambao upo Mahakamani; ufilisi wa makampuni; utekelezaji wa amri za Mahakama za ndani na nje ya nchi; miko ya uongozi na utumishi wa umma na Sheria za Utumishi wa Umma pamoja uendeshaji wa mashauri.

Mada nyingine ni migogoro ya utumishi wa Umma, sheria za ununuzi wa Umma; usuluhishi katika mikataba ya ujenzi; usuluhishi wa ndani na kimataifa, Sheria ya Ardhi na mikopo kupitia Ardhi; Mashauri ya marejeo ya Mahakama; Uendeshaji wa mashauri ya Rufaa katika Mahakama ya Rufaa, uendeshaji wa mashauri ya kodi na mashauri ya haki za binadamu kitaifa na kimataifa.

Akifunga mafunzo hayo Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro aliwataka Mawakili wa Serikali kuwa chachu katika utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano, maridhiano na usuluhishi kutokana na elimu na stadi za utatuzi wa migogoro kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.

Dkt. Ndumbaro aliwataka pia kuendelea kupunguza idadi ya mashauri ya madai na usuluhishi yanayofunguliwa na yanayoendelea kwa kuyamaliza kwa njia ya majadiliano, maridhiano na usuluhishi hivyo kuimarisha juhudi za Serikali katika kuvutia wawekezaji na kutekeleza miradi mbalimbali nchini.



*Baadhi ya Mawakili wa Serikali wakimsikiliza Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo (hayupo pichani) wakati akifungua mafunzo ya Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha.*




Prof. Florens Luoga

**Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania akiwasilisha mada inayohusu Utatuzi wa Migogoro kwa njia ya Majadiliano kwa Mawakili wa Serikali**

# MAWAKILI FANYENI UTAFITI KABLA YA MAJADILIANO YA MIGOGORO

> ***Kabla ya kuingia katika majadiliano lazima Wakili ujue dhumuni la kufanya majadiliano na kuangalia kama ndiyo njia nzuri ya kufikia muafaka kwa kuwa lengo kuu la majadiliano ni kufanikiwa.***
>
> *Alisema Prof. Luoga*

Gavana wa Benki kuu ya Tanzania, Prof. Florens Luoga amewataka Mawakili wa Serikali kufanya utafiti kabla ya kwenda kwenye majadiliano ili kujua dhumuni la kufanya majadiliano na kuona kama majadiliano hayo ndiyo njia nzuri ya kufikia muafaka na kujua kesi vizuri, ubora na udhaifu uliopo.

Prof. Luoga aliyasema hayo jijini Arusha wakati akiwasilisha mada ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano kwenye mafunzo ya Mawakili wa Serikali yaliyoandaliwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

“Kabla ya kuingia katika majadiliano lazima Wakili ujue dhumuni la kufanya majadiliano na kuangalia kama ndiyo njia nzuri ya kufikia muafaka kwa kuwa lengo kuu la majadiliano ni kufanikiwa”, alisema Prof Luoga.

Alieleza kuwa mshiriki wa majadiliano lazima ajue hali ya upande wenu, dhumuni la majadiliano kwa upande wenu na katika upande mwingine lazima ujue kesi yako vizuri, ubora na udhaifu uliopo.

Prof. Luoga alieleza kuwa kuna hatua kuu mbili ambazo ni kuweka mikakati (Planning Stage) na maafikiano (Bargaining Stage) ambapo washiriki wa majadiliano wanapaswa kutambua hali inayopelekea majadiliano kuwa njia sahihi ya kupata suluhishi.

Alifafanua kuwa katika kuweka mikakati washiriki wa majadiliano wanapaswa kutambua wakati sahihi wa

kupendekeza kufanyika kwa majadiliano na mhusika anapaswa kutengeza mazingira ambayo upande wa pili utaona majadiliano ni njia sahihi.

Prof. Luoga alieleza kuwa katika hatua hii kiongozi anapaswa kuandaa timu itakayoshiriki majadiliano, rasilimali (Resources/ Experts), kutambua watu wenye uwezo ambao watasaidia katika kufanikisha majadiliano, kuzingatia taaluma maalumu, na kuiweka sawa timu nzima.

Kwa upande wake, Wakili wa Serikali Careen Masonda alishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuandaa mafunzo ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi kwa sababu mafunzo hayo yanawaongezea ufanisi katika majukumu yao ya kazi ya kila siku katika kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi.

"Tumefundishwa na mwezeshaji mwenye uzoefu, ujuzi na aliyefanya majadiliano kwa niaba ya Serikali kwa muda mrefu. Mafunzo aliyotupa yamekuwa ni ya vitendo (very practical) tofauti na yale tuliyokuwa tunayajua ambayo mara nyingi ni ya kitaaluma zaidi na kupata nafasi ya kujua uhalisia wa kile kinachojiri kwenye mazungumzo," alisema Masonda.

Masonda alisema kuwa wameweza kujifunza mbinu za kufanya majadiliano yatakayoleta tija zaidi kwa Serikali, mfano mzuri ni jinsi ya kuchagua timu ya kufanya majadiliano (negotiation team), kuandaa dodoso la majadiliano (negotiation brief), na nini cha kufanya kabla na wakati wa mazungumzo.

Alitoa mfano wa shauri la tarehe 24/03/2022 la Exim Bank Limited dhidi ya Tanzania Fertilizer ambapo Serikali ilifanikiwa kufanya majadiliano katika shauri hilo lililokuwa na madai ya dola za Marekani milioni sita na laki saba.

Katika majadaliano hayo mdai alikubali kulipwa dola za Marekani milioni mbili na laki saba tu na kusaidia kupunguza madai hayo kutoka dola za Marekani milioni 6 na laki 7 hadi dola za Marekani milioni 2 na laki 7. Hivyo, kusaidia kuokoa dola za Marekani milioni nne ambazo Serikali ingepaswa kuzilipa endapo shauri hili lingeendelea kuendeshwa Mahakamani.



*Baadhi ya Mawakili wa Serikali wakisikiliza mada iliyowasilishwa na Prof. Florens Luoga, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (hayupo pichani) akiwasilisha mada kuhusu kufanya utafiti kabla ya majadiliano ya migogoro wakati wa mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika jijini Arusha.*




Mhe. Zahra Maruma

**Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania akiwasilisha mada inayohusu Uendeshaji wa Usuluhishi Uliopo Mahakamani**

# UENDESHAJI WA USULUHISHI ULIOPO MAHAKAMANI

Kanuni ya VIII Kanuni Ndogo ya 26 ya Sheria ya Mienendo ya Mashauri ya Madai (Civil Procedure Code) inaeleza dhumuni la dhana nzima ya usuluhishi na jinsi Mahakama katika kuzingatia haki inatolewa kwa wakati basi mashauri yanapaswa kupitia katika usuluhishi kama moja ya njia ya kufikia muafaka katika utoaji haki.

Kauli hiyo ilitolewa na Mhe. Zahra Maruma, Jaji wa Mahakama Kuu Tanzania wakati wa mafunzo ya Mawakili wa Serikali na kusema kuwa katika kuendesha usuluhishi, Mahakama imejiwekea mkakati wa kuwa huru kabisa na kutojikita kabisa na taratibu za kisheria ili kuweza kuwafanya wadaiwa kuwa huru na kushiriki vyema katika kufikia suluhu.

Mhe. Maruma alisema Mahakama inatumia hatua nne ambazo ni kufungua kikao cha usuluhishi, kupata taarifa kutoka pande zote kwa pamoja, kukaa na upande mmoja (private session), majadiliano na kukamilisha usuluhishi.

“Wakili wa Serikali anapaswa kujua nafasi yake na kujua hatua za usuluhishi, kujua mgogoro uliopo, anapaswa kuwa na utayari wa usuluhishi, kuwa na mbinu za kujadili, kujua hoja zilizopo katika mgogoro na kuwa na utayari wa usuluhishi kwa kuzingatia mawasiliano mazuri yaliyopo kati yake, Ofisi yake pamoja na mteja anayemwakilisha,” alisema Mhe Maruma.

Alifafanua kuwa changamoto nyingi kwenye usuluhishi zinatokana na Mawakili wa Serikali kutokuwa na ufahamu wa hatua za usuluhishi, washiriki kuwa na uzoefu mdogo katika usuluhishi, mtazamo hasi katika usuluhishi na

kutokuwa na utayari wa kufanya usuluhishi.

Jenipher Kaaya, Wakili wa Serikali Mfawidhi, Dodoma alisema mafunzo hayo yatawajengea uwezo, weledi na kujiamini kwenye meza ya usuluhishi Mahakamani na kuzingatia haki inatolewa na kufikia muafaka kwa wakati ili kupunguza idadi ya mashauri katika mahakama.

Kaaya alisema kuwa mada ya uendeshaji wa mashauri ya usuluhishi yaliyopo mahakamani ina lengo la kutambua umuhimu wa Mawakili wa Serikali kuzingatia usuluhishi kama njia mojawapo ya kufikia muafaka wa utoaji haki kwa wakati na kupunguza gharama za uendeshaji wa mashauri ya taasisi zao mahakamani.

“Sisi kama Mawakili wa Serikali tunatakiwa kuzijua hatua zote nne ambazo Mahakama inazitumia katika kuendesha mashauri ya usuluhishi uliopo mahakamani ili tuweze kupunguza mashauri yaliyopo mahakamani yanayozikabili taasisi zetu”, alisema Kaaya

"Hivyo, ni Imani yangu kuwa mafunzo haya yatatujengea uwezo wa kuendesha mashauri ya usuluhishi yaliyopo mahakamani kwa kushirikisha pande zote mbili bila kuegemea upande wowote ili kuhakikisha mashauri yanaisha kwa wakati, kwa amani na haki stahiki inapatikana" alisema Kaaya.

> ***Wakili wa Serikali anapaswa kujua nafasi yake na kujua hatua za usuluhishi, kujua mgogoro uliopo, anapaswa kuwa na utayari wa usuluhishi, kuwa na mbinu za kujadili, kujua hoja zilizopo katika mgogoro na kuwa na utayari wa usuluhishi kwa kuzingatia mawasiliano mazuri yaliyopo kati yake, Ofisi yake pamoja na mteja anayemwakilisha.***
>
> Mhe. Zahra Maruma
> **Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania**



*Wakili wa Serikali Mwandamizi Jenipher Kaaya akisikiliza mada ya uendeshaji wa usuluhishi uliopo mahakamani iliyowasilishwa na Mhe. Zahra Maruma Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania (hayupo pichani) wakati wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha.*




Juma Kisongo

**Meneja Masuala ya Bodi na Utawala Huduma za Sheria, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) akiwasilisha mada inayohusu Utatuzi wa Migogoro ya Kodi Nchini Tanzania**

# MFUMO WA UTATUZI WA MIGOGORO YA KODI NCHINI TANZANIA

Kodi ni mchango wa lazima kutoka kwa mwananchi au kampuni ya kibiashara kwa lengo la kugharamia matumizi ya Serikali na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ndiyo imepewa nguvu kwa mujibu wa kifungu cha 5 (1) cha Sheria ya Ukusanyaji wa Mapato ya kusimamia na kuhakikisha kuwa sheria inatumika ipasavyo katika kukusanya mapato.

Kauli hiyo ilitolewa na Dkt. Boniphace Luhende, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, na Juma Kisongo, Meneja Masuala ya Bodi na Utawala Huduma za Sheria, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wakiwasilisha mada wakati wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha.

Wawezeshaji waligusia masuala mbali mbali ikiwemo maana ya kodi, migogoro ya kodi, sheria zinazosimamia masuala ya kodi, taratibu za usimamizi wa kodi, njia za utatuzi wa migogoro ya kodi, mamlaka za kusikiliza migogoro ya kodi, maamuzi ya kikodi, taratibu za kukata rufaa za kodi na utekelezaji wa maamuzi ya kikodi.

Wakufunzi walieleza kuwa migogoro hii ya kodi ni ile inayotokana na ukusanyaji wa kodi kwa walipa kodi. Migogoro huanza pale TRA inapokadiria kiasi fulani cha kodi ya Serikali na mlipa kodi kutokuridhika na kiwango hicho kwani kwa maoni ya mlipa kodi ni kikubwa au hakustahili kulipa kodi husika.

Walieleza kuwa Tanzania ina sheria mbalimbali za kodi ikiwamo Sheria ya Kodi ya Mapato (The Income Tax Act); Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tanzania Revenue Authority Act);

Sheria ya Ongezeko la Thamani (The Value Added Tax Act); Sheria ya Ushuru wa Stempu (Stamp Duty Act) na sheria nyingine.

"Pale ambapo mlipa kodi hajaridhika na maamuzi ya kodi, kuna mamlaka nne nchini Tanzania zenye uwezo ya kutatua migogoro ya kikodi. Mamlaka hizo ni; Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; Bodi ya Rufaa ya Kodi (TRAB); Baraza la Rufaa la kodi (TRAT); na Mahakama ya Rufani (CAT)" alieleza Kisongo.

Maamuzi ya kikodi yanayoweza kuwasilishwa kwenye mamlaka hizo ni kama vile tathmini (assessment), maelekezo, ushauri (opinion) na hukumu. Maamuzi yoyote ya kikodi yanakatiwa rufaa kwenye mamlaka husika kama ilivyoanishwa kwenye sheria na rufaa hiyo lazima ipelekwe ndani ya muda husika kwa mujibu wa sheria. Vile vile, ilielezwa kuwa maamuzi ya mashauri ya kikodi hutekelezwa kama maamuzi ya mashauri mengine na yanatakiwa yatekelezwe ndani ya muda wa siku thelathini.

Aidha, wakufunzi walisisitiza umuhimu wa ulipaji wa kodi kwa maendeleo ya nchi na kuhimiza wananchi na taasisi zote ikijumuisha za Serikali kulipa kodi kama inavyotakiwa kisheria.

***"Pale ambapo mlipa kodi hajaridhika na maamuzi ya kodi, kuna mamlaka nne nchini Tanzania zenye uwezo ya kutatua migogoro ya kikodi. Mamlaka hizo ni; Kamishina Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; Bodi ya Rufaa ya Kodi (TRAB); Baraza la Rufaa la kodi (TRAT); na Mahakama ya Rufani (CAT)."***

Juma Kisongo

**Meneja Masuala ya Bodi na Utawala Huduma za Sheria, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)**




*Baadhi ya Mawakili wa Serikali wakisikiliza mada ya utatuzi wa migogoro ya kodi iliyowasilishwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende (hayupo pichani) wakati wa mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika jijini Arusha.*




Prof. Ninatubu Lema

**Mjumbe wa Bodi ya PPRA akiwasilisha mada inayohusu Utatuzi wa Migogoro katika Mikataba ya Ujenzi**

# USULUHISHI, USIMAMIZI NA UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA MIKATABA YA UJENZI

Miradi ya ujenzi nchini Tanzania kwa ujumla imekuwa ikigharimu kiasi kikubwa cha fedha na imekuwa ni changamoto na huchukua muda mrefu kukamilika na hivyo kupelekea migogoro mingi kuibuka baina ya Serikali na wakandarasi.

Prof. Ninatubu Lema alitoa kauli hiyo kwenye mafunzo ya Mawakili wa Serikali na kusema baadhi ya hatari hazionekani na zingine zinaonekana ambazo zinajumuishwa kwenye mikataba na tunapaswa kuweka nguvu kubwa katika miradi mikubwa ya ujenzi.

"Takwimu inayotarajiwa kuwa bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2022/23 ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pekee ni kiasi cha shilingi trilioni 3.727 kwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo inaweza kuwa na hatari kwenye mikataba itakayoingiwa", alisema Prof. Lema.

Alitoa mfano wa mikataba ya miradi mikubwa kama wa ujenzi wa bwawa la umeme la Julius Nyerere na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) ambayo inapaswa kuwekewa nguvu nyingi katika kusimamia hatari zinazoonekana ambazo zimejumuishwa kwenye mikataba na kutoa njia za jinsi ya kuzishughulikia.

Prof. Lema alieleza kuwa mchakato wa kushughulikia hatari unaweza kusababisha wahusika kutokuwa na makubaliano juu ya majukumu ya kimkataba juu ya hatari na wakati mwingine kusababisha migogoro.

Alieleza kuwa hakuna kikomo cha aina za migogoro inayoweza kutokea wakati wa utekelezaji wa kazi. Kwa ujumla, migogoro mingi hutokana na uamuzi wa madai, uthibitisho wa malipo; maelekezo (au ukosefu wake), maoni au tathmini kwa mpangilio huo.

"Mgogoro unaweza kutokea wakati mkandarasi au mwajiri hakubaliani na

uamuzi wa mhandisi ama kwa ukweli au kiasi au ikiwa mhandisi hatajibu ndani ya muda ulioainishwa katika mkataba", aliongeza Prof Lema.

Tumsifu Ilomo, Wakili Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya alifurahishwa na namna mtoa mada alivyowasilisha na kusema itakwenda kuwasaidia katika mikataba ya ujenzi wanayoisimamia hasa katika ujenzi wa barabara, vituo vya afya, hospitali za Wilaya, na mikataba ya manunuzi inayofanyika katika Ofisi zao.

"Baadhi ya mikataba tunayoingia hasa kwenye Halmashauri zetu inakosa masharti ya msingi kama vile muda wa utekelezaji wa mkataba, gharama za mkataba, namna malipo yatakavyofanyika, muda wa kuanza kutekeleza mkataba, na kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi na hivyo kuzifanya Halmashauri kuingia kwenye migogoro ambayo tungeweza kuikwepa kama tungezingatia usimamizi mzuri wa mikataba yetu," alisema Ilomo.

Ilomo aliongeza kuwa Mawakili watakuwa wamepata uelewa na kuandaliwa vizuri ili kutekeleza majukumu yetu vizuri ndani na nje ya nchi na kuweza kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi katika mafunzo haya.

*"Mgogoro unaweza kutokea wakati mkandarasi au mwajiri hakubaliani na uamuzi wa mhandisi ama kwa ukweli au kiasi au ikiwa mhandisi hatajibu ndani ya muda ulioainishwa katika mkataba."*

Prof. Ninatubu Lema

**Mjumbe wa Bodi ya PPRA**




*Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa kwenye picha ya pamoja na Mgeni Rasmi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Mary Makondo (aliyeketi katikati) baada ya kufungua Mafunzo ya Mawakili wa Serikali jijini Arusha.*




Dkt. Clement Mashamba

**Mhadhiri Mwandamizi wa Shule ya Sheria kwa Vitendo akiwasilisha mada inayohusu Uendeshaji wa Mashauri ya Haki za Binadamu**

# UENDESHAJI WA MASHAURI YA HAKI ZA BINADAMU

Haki za Binadamu ni haki ambazo mtu anazipata mara tu anapozaliwa, na anaendelea kuwa nazo hadi kifo chake.

Akiwasilisha mada kwenye mkutano wa Mawakili wa Serikali kuhusu uendeshaji wa mashauri ya Haki za Binadamu katika Mahakama za ndani, Dkt. Clement Mashamba, Mhadhiri Mwandamizi wa Shule ya Sheria kwa Vitendo alisema kuwa haki za binadamu ni haki ambazo mtu anazipata mara tu anapozaliwa, na anaendelea kuwa nazo hadi kifo chake.

"Kwa maneno mengine, kitendo cha kuzaliwa ukiwa mwanadamu na si kiumbe kingine kinakupa moja kwa moja haki ambazo viumbe vingine hawana" alisema Dkt Mashamba.

Dkt. Mashamba alisema kuwa mada hii ina umuhimu mkubwa sana hasa ukizingatia kwamba Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inawajibika kuiwakilisha Serikali katika mashauri ya Haki za Binadamu yanayofunguliwa katika Mahakama za ndani, Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu ya Afrika, Kamisheni ya Haki za Binadamu na Watu ya Afrika pamoja na Kamati ya Wataalamu ya Afrika ya Haki na Ustawi wa Mtoto kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Akizungumzia kuhusu umuhimu wa kufahamu namna bora ya kuandaa na kuendesha Mashauri kuhusu Haki za Binadamu, Dkt. Clement Mashamba alisema kupitia Shauri Na. 9 la Mwaka 2016 lililofunguliwa na Rashid Adil na wenzake dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wenzake katika Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, waliokuwa wanapinga uwepo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema shauri hili ni kielelezo tosha kitakachowasaidia Mawakili wa Serikali kujifunza namna bora ya kuiwakilisha na kuandaa utetezi wa Serikali na uwepo wa maslahi mapana

katika mashauri ya Haki za Binadamu na hivyo kuisaidia Serikali kupata ushindi katika mashauri mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mada hiyo ilitoa mtazamo chanya wa Mahakama kwa mashauri ya Haki za Binadamu na hususani uwakilishi unaofanywa na Mawakili wa Serikali katika kutetea Serikali kupitia mada iliyoandaliwa na Mhe. Dkt. Benhajj Masoud Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania na Mkuu wa Shule ya Sheria kwa Vitendo.

Pamoja na mambo mengine, mafunzo haya yalilenga kujifunza namna ambavyo kuna uhusiano mkubwa wa Haki za Binadamu zinazotajwa katika Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu ambayo imeridhiwa na Tanzania pamoja na Haki za Binadamu zilizoorodheshwa katika Ibara ya 12 mpaka ya 29 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Jaji Benhajj Masoud alirejea shauri la Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Dickson Sanga, Shauri la Rufaa Na. 175 la Mwaka 2021 ambalo lilitokana na hukumu ya Mahakama Kuu kuwa zuio la dhamana kwa baadhi ya makosa ni kinyume cha Haki za Binadamu katika Katiba. Shauri hili lilitukumbusha mbinu zilizotumiwa na Mawakili kuhakikisha wanaiwakilisha vyema Serikali katika Rufaa na kushinda kwa kuonesha uwepo wa uwiano wa Haki za Binadamu na wajibu katika Katiba.

Mada hii ni muhimu ukizingatia kwamba mashauri yanayohusisha Haki za Binadamu yana maslahi mapana na uendeshaji wake unahitaji umakini sana. Aidha, uzoefu wa watoa mada katika mifumo ya Mahakama za ndani na za Kimataifa umeongeza ufanisi katika nyenzo za ufundishaji na maeneo ya kutilia mkazo. Hivyo, ni wito wangu kwamba mada hii ni muhimu kuendelea kutolewa kwa Mawakili wa Serikali kutokana na uwepo wa mashauri mbali mbali yanayohusu Haki za Binadamu mathalani mashauri kuhusu kuondolewa kwa wananchi wanaoishi ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro na Pori Tengefu la Loliondo.

Akizungumza kwa niaba ya Mawakili wa Serikali walioshiriki mafunzo hayo, Wakili wa Serikali Bw. Stanley Kalokola alisema kuwa mafunzo hayo ni muhimu sana kwao kwa kuwa kupitia mafunzo hayo kutawaongezea uzoefu katika uandaaji wa utetezi na mbinu mbalimbali za kuweza kuiwakilisha Serikali kwa ufanisi kwenye mashauri yanayohusu Haki za Binadamu katika Mahakama mbalimbali nchini.

Aliongeza kuwa kama Mawakili wa Serikali wanatambua kwamba pamoja na kuitetea Serikali, pia wanao wajibu wa kuishauri Serikali juu ya masuala ya Haki za Binadamu. Hivyo, mafunzo haya yamewaongezea uelewa na nyenzo mbalimbali kuhusu masuala ya Haki za Binadamu pamoja na jinsi mifumo yake inavyofanya kazi kwa kuwa Serikali katika utekelezaji wake wa majukumu ya wananchi inawajibika kuzingatia misingi mbalimbali ya Haki za Binadamu.




Mhe. Dkt. Benhajj Masoud

**Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania na Mkuu wa Shule ya Sheria kwa Vitendo**

# WATUMISHI WAANDALIWA KUWA VIONGOZI MAHIRI



*Mhe. Balozi Ombeni Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Uongozi (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kutoa mafunzo kuhusu uongozi kwa viongozi hao yaliyofanyika jijini Dar es Salaam. Wa pili kushoto ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende.*

**"Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inatakiwa kuwa Ofisi ya kutengeneza viongozi, tunawaandaa ili wajaze nafasi katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na katika ofisi nyingine za Serikali." alisema Dkt. Luhende.**

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kuandaa mafunzo ya watumishi yenye lengo la kuwajengea uwezo na kuwaandaa kuwa viongozi wa baadae kwa manufaa ya Taifa ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija Luhende wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kwa Serikali inatakiwa kuwa Ofisi ya kutengeneza viongozi ndio maana tunawatengeneza kwa maana kwamba tunawaandaa ili wajaze nafasi katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na katika ofisi nyingine za Serikali", alisema Dkt. Luhende.

Aliongeza kuwa mafunzo ni muhimu kwa taifa zima kwa sababu viongozi wanaoandaliwa watasaidia kujaza nafasi mbalimbali katika taasisi nyingine za Mkuu wa Serikali, kwa hiyo lazima tuwatengeneze", alisema Dkt. Luhende.

Alisema kuwa jambo hili la utoaji wa mafunzo lilipata msukumo zaidi katika Sekta ya Sheria kwenye taarifa kadhaa ikiwemo taarifa ya Mhe. Pius Msekwa tangu miaka ya sabini, lakini pia kupitia taarifa ya Mhe. Jaji Mark Bomani ya mwaka 1994 ambapo zinasema kuwa Sekta ya Sheria imekuwa na changamoto ya kutokuandaa




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende akifungua mafunzo ya uongozi yaliyofanyika kwa muda wa siku tatu kwa viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali(hawapo pichani) yaliyotolewa na Wakufunzi wa Taasisi ya Uongozi yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.*

viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yenye lengo la kuwajengea uwezo viongozi katika kuhakikisha wanatekeleza majukumu ipasavyo kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Kanuni za Utumishi wa Umma.

"Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambazo zinahitaji viongozi kwa kuwa kule kuna wakurugenzi wa idara za Sheria au wakuu wa vitengo vya Sheria.

"Maono yangu ni kwamba baada ya miaka mitano basi nikienda huku nikute kuna mtu alitoka Ofisi ya Wakili viongozi kwa kuzingatia ukweli kuwa tunao Mawakili wazuri mno lakini hatuwaandai kuwa viongozi wa baadae.

Dkt. Luhende alisema ipo haja ya kujifunza namna bora ya kutekeleza majukumu hivyo wale Mawakili wa

Serikali Wakuu pamoja na Waandamizi naomba kuwaeleza kuwa ninyi ni viongozi hata kama hamna nafasi za kimadaraka kwa mujibu wa muundo mnao watumishi mnaowasimamia.

Dkt. Luhende alisema yapo mambo mengi wanayotarajia na miongoni mwake ni namna bora ya kupanga kazi zao, usimamizi bora na utoaji wa taarifa kwa kila kazi mnazofanya na kuzisimamia kama viongozi.

Alisema kuwa viongozi wana wajibu wa kusimamia watumishi walio chini yao, hivyo kama viongozi wanapaswa kutekeleza majukumu mawili ambayo ni jukumu la kitaaluma kwa kuwa ni lazima waende Mahakamani kuendesha mashauri la pili kama kiongozi ni kusimamia vizuri wale waliochini yako.

Dkt. Luhende alisema namna bora ya kujipima kutokana na malengo tuliyojiwekea lazima tujue mambo gani ambayo tulifikiria tunapaswa kuyafanikisha, hivyo tunapomaliza mwaka lazima tujipime kama tumetekeleza malengo na hilo ndiyo kusudi la mafunzo ya kutuwezesha kuwa na stadi za kufanya tathmini na kujipima.

Alisema namna bora ya kusimamia wale walio chini yao ni kuwasiliana, kuzingatia muda katika kutekeleza majukumu yao, usimamizi na uendeshaji wa vikao, maadili ya uongozi, usimamizi wa viashiria hatarishi, na usimamizi wa rasilimali fedha na rasilimali watu.

Aidha, Dkt. Luhende aliwasisitiza viongozi kuwa wanapaswa kufahamu pamoja na kazi nyingi walizonazo kama viongozi wanao wajibu wa kutekeleza majukumu mengine ya kiuongozi wanayopangiwa kwa manufaa mapana ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na taifa kwa ujumla.

Nao viongozi walioshiriki mafunzo hayo wakiongea kwa nyakati tofauti waliushukuru uongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuandaa mafunzo ya uongozi kwa kuwa yamewapatia fursa ya kukumbushana mambo mbalimbali ambayo yatawasaidia kuboresha utendaji wao wa kila siku katika kutekeleza majukumu yao.



*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walioshiriki mafunzo ya uongozi wakisikiliza mada zilizowasilishwa na wataalamu wa Taasisi ya Uongozi (hawapo pichani) yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.*




*Mhe. Balozi Ombeni Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Uongozi akitoa mada kuhusu uongozi kwa viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hawapo pichani) yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiongea katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Mei Mosi, 2022 yaliyofanyika jijini Dodoma.* ***Picha kwa hisani ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu.***

# RAIS SAMIA: NITABORESHA MASLAHI YA WAFANYAKAZI NCHINI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ameahidi kuboresha maslahi ya watumishi nchini kwa lengo la kuinua hali zao za kiuchumi ili waweze kumudu gharama za maisha.

Mheshimiwa Rais alitoa ahadi hiyo wakati akizungumza na watumishi mbalimbali waliojitokeza katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliyofanyika kwenye viwanja vya Jamhuri Jijini Dodoma.

Katika kuhakikisha ahadi hiyo inatekelezeka, Rais Samia aliagiza kufanyika kwa majadiliano yatakayokuwa na lengo la kuimarisha maslahi ya wafanyakazi kati ya Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) na Serikali ili kujua kiwango stahiki cha maslahi kinachohitajika kuongezwa.

"Serikali imeshaunda Bodi za kima cha chini cha mshahara kwa sekta zote yaani sekta binafsi na ile ya umma na tayari zimeshaanza kufanyia kazi tathimini ya mishahara iliyopo sasa ili kujua ni kiwango gani kinatakiwa kuongezwa", alisema Mhe. Rais.

Aidha, Mhe. Rais aliagiza Maafisa Rasilimali Watu kwa kushirikiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kushughulikia mapema haki na stahiki za watumishi wanaotarajia kustaafu ndani ya miezi sita ili mtumishi anapofika muda wa kustaafu mafao yake yawe tayari yametoka hatua itakayosaidia kuondoa usumbufu miongoni mwa wastaafu nchini.

Akizungumzia watumishi waliofanya kazi kwa muda

mrefu na kisha kufukuzwa kazi kwa sababu ya vyeti feki, Mhe. Rais ameiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kushughulikia stahiki zao zinazotokana na makato ya mishahara yao ili waweze kulipwa kwa kuwa Serikali inatambua mchango wao walioutoa kipindi walichotumikia Taifa.

Kuhusu namna Serikali ilivyoendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa umma kote nchini, Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan amesema kuwa Serikali imeendelea kustawisha maslahi ya wafanyakazi tangu mwaka 2021 ikiwepo kupunguza makato ya kodi; kuongeza umri wa wategemezi kutoka miaka 18 mpaka 21; kupandisha vyeo vya watumishi; kubadilisha kada; kulipa malimbikizo ya mishahara kwa watumishi pamoja; na kutoa ajira mpya zilizosaidia kujaza nafasi mbalimbali zilizokuwa wazi na hivyo kuongeza ufanisi katika maeneo mbalimbali nchini.

Nayo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilishiriki maadhimisho hayo ikiongozwa na Mwenyekiti wa TUGHE, tawi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mtani Songorwa ambapo waliungana na watumishi kutoka sehemu mbalimbali nchini kushiriki maadhimisho hayo kwa maandamano yaliyopita mbele ya Mgeni Rasmi wakiwa na mabango yenye ujumbe unaolenga kuonyesha mshikamano baina ya watumishi, Vyama vya Wafanyakazi na Serikali yakisindikizwa na kauli mbiu isemayo "Mishahara na Maslahi Bora kwa wafanyakazi ndio Kilio chetu: Kazi iendelee".

> **"Serikali imeshaunda Bodi za kima cha chini cha mshahara kwa sekta zote yaani sekta binafsi na ile ya umma na tayari zimeshaanza kufanyia kazi tathimini ya mishahara iliyopo sasa ili kujua ni kiwango gani kinatakiwa kuongezwa."**
>
> **Mhe. Rais Samia**



*Wafanyakazi mbalimbali waliojitokeza katika kiwanja cha Jamhuri kilichopo jijini Dodoma kushiriki Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Mei Mosi, 2022.* ***Picha kwa hisani ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu.***



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dkt. Allan Kijazi (kulia) na Mkurugenzi wa Kampuni ya Tanzania Plantations Ltd wakionesha hati ya makubaliano ya makabidhiano ya mashamba ya Kampuni ya Tanzania Plantantions na Serikali wilayani Arumeru mkoani Arusha. Wa pili kulia ni Waziri wa Wizara hiyo, Mhe. Angelina Mabula (Mb).* ***Picha kwa hisani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.***

# SERIKALI YAKABIDHIWA MASHAMBA YA TANZANIA PLANTATIONS LTD

Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kurudisha mashamba yenye ukubwa wa ekari 6,176.5 yaliyokuwa yanamilikiwa na Tanzania Plantations Ltd yaliyopo Wilaya ya Arusha na Arumeru baada ya kumalizika kwa mgogoro wa muda mrefu.

Mashamba hayo yalikuwa yanajulikana kama Karangai Estate na Lucy Estate ambapo mnamo tarehe 6 Julai, 1999 na tarehe 6 Desemba, 1999 Serikali ilibatilisha baadhi ya mashamba yenye hati miliki Na. NP. 304, NP. 305, NP. 373, NP. 427, CT. 5189, CT. 8374 ambayo mmiliki alikiuka masharti ya umiliki.

Mgogoro kati ya Kampuni ya Tanzania Plantations Ltd na Serikali uliibuka mwaka 1999 baada ya kampuni hiyo kupinga ubatilisho wa mashamba yake uliofanywa na Serikali kutokana na kampuni hiyo kushindwa kutimiza masharti ya umiliki jambo lililoifanya kufungua kesi Mahakama Kuu Kanda ya Arusha mwaka 2015.

Kampuni ya Tanzania Plantations Ltd ilifungua kesi Na. 50 ya mwaka 2015 katika Mahakama Kuu ya Tanzania Arusha na kumshtaki Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali akidai Mahakama itamke kwamba ubatilishaji wa mashamba yake yenye Hati NP 304, 305, 9626, 8374 na 5159 yaliyoko Arumeru Mkoa wa Arusha

yenye ukubwa wa takribani ekari 10, 146 ulikuwa batili.

Mwaka 2019 Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliwasilisha ombi la kufanya majadiliano na mdai kwa lengo la kumaliza shauri nje ya Mahakama ambapo Mahakama iliridhia pande mbili za shauri kumaliza suala hilo nje ya Mahakama.

Katika makubaliano ya kutafuta suluhu nje ya Mahakama, Serikali ilikubali kulipa shilingi bilioni 5.7 kwa ajili ya fidia ya mashamba Na. 304 na Na. 305 Nduruma yenye ukubwa wa ekari 16,133 na shamba la ekari 43.5 ambalo halikubatilishwa lakini ilionekana ni busara likachukuliwa na Serikali. Pia, Serikali ililipa fidia ya mkonge na mtambo wa kuchakata mkonge uliokuwa ukifanya kazi.

Tarehe 29 Aprili, 2022 Kata ya Bwawani Wilaya ya Arumeru yalifanyika makabidhiano ya mashamba baina ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dkt. Allan Kijazi na Mkurugenzi wa Tanzania Plantation Ltd ndugu Ladhia Prabhudas Pradip mbele ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Dkt. Angeline Mabula.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Dkt. Angeline Mabula alisema, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan aliridhia makubaliano yafanyike na kutoa fedha kwa ajili ya fidia ili kumaliza mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu.

Dkt. Mabula alimshukuru Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa busara na hekima ya kuona uhitaji wa kuwa na mazungumzo na Tanzania Plantation Ltd lakini pia akiangalia mustakabali wa watu waliokuwa eneo hilo na kuelekeza makubaliano yafanyike na akatoa fedha za fidia kwa mmiliki.

Kwa mujibu wa Dkt. Mabula alisema, Serikali ya Mhe. Rais Samia haiwezi kuwatelekeza wananchi waliokuwa wakiishi katika mashamba hayo na kubainisha kuwa itaweka utaratibu mzuri ili wananchi hao waweze kufaidika na matunda ambayo Serikali imepanga.

Dkt. Mabula aliagiza halmashauri ambazo ni mamlaka za upangaji miji nchini kuendelea kufanya tathmini kwa yale mashamba ambayo wamiliki wake wameshindwa kuyaendeleza au kuyatelekeza hatua za kuyatwaa zianze kufanyika mara moja.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John Mongela aliwataka wananchi kuendelea kusubiri utaratibu wa matumizi ya mashamba hayo utakapotolewa. Aidha, aliwatahadharisha kuwa mashamba hayo bado ni mali ya Serikali.

Aliwaonya kutofanya eneo hilo kuwa shamba la bibi na kuwakemea baadhi ya viongozi ambao ndio vinara namba moja katika kuanzisha migogoro na kuwataka viongozi wa vijiji na vitongoji kutokuwa madalali bali watimize wajibu wao wa kusimamia wananchi na mali zao na sio kuanzisha migogoro.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dkt. Allan Kijazi alisema, Wizara yake kwa kushirikiana na Wizara na taasisi nyingine imeanza kuchukua hatua zitakazoiwezesha Serikali kufanya maamuzi kuhusu matumizi ya mashamba hayo ikiwemo uvunaji wa mkonge kwa kuzingatia baadhi ya mahitaji ya wananchi.

Dkt. Kijazi alisema Serikali imeweka pia utaratibu wa ulinzi wa mashamba sambamba na mamlaka ya Mkoa ya kusimamia mali kipindi hiki ambacho mpango wa matumizi ya ardhi unaandaliwa na aliwataka wananchi kutoa ushirikiano.

Naye Kamishna wa Ardhi nchini Nathaniel Methew Nhonge alisema, baada ya makabidhiano ya shamba yaliyofanyika sasa ni lazima eneo hilo liandaliwe mpango wa matumizi ya ardhi kwa ajili ya manufaa ya nchi na kusisitiza kuwa zile changamoto zitakazojitokeza zitafanyiwa kazi na kutafutiwa ufumbuzi.

Kwa upande wake, Wakili wa kampuni ya Tanzania Plantation, Alute Mughwai aliishukuru Serikali kwa kuweza kukubaliana na kumaliza mgogoro huo kwa njia ya maridhiano na kuwa maridhiano hayo yamewezesha mgogoro huo kumalizika kwa amani.

Wakili Mughwai aliishukuru Serikali kwa kumaliza suala hilo kwa amani na kuiachia Serikali suala la mipango ya matumzi ya ardhi na kusema mteja wake alikuwa anaomba jambo hili limalizike mapema.



# MAHAKAMA YAAMURU WABUNGE 19 WA CHADEMA KUENDELEA NA UBUNGE

Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imeridhia wabunge 19 wa Viti Maalum waliovuliwa uanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuendelea kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania mpaka pale Mahakama itakaposikiliza shauri lao la msingi tarehe 13 Juni, 2022.

Uamuzi huo ulitolewa tarehe 16 Mei, 2022 na Jaji anayesikiliza shauri hilo Mhe. John Mgeta wakati shauri hilo lilipoitwa kwa mara ya kwanza kwa ajili ya kutajwa Mahakamani hapo.

Ombi hilo Na. 13 la mwaka 2022 ni ombi dogo kwenye shauri la msingi namba 16 la mwaka 2022 ambapo Wabunge hao wakiongozwa

na Mhe. Halima James Mdee, wanaiomba Mahakama kuwarejeshea uanachama wao baada ya Kamati Kuu ya Chama hicho kuamua kuwavua ubunge wanachama hao 19, uamuzi ulioridhiwa na Baraza Kuu mpaka pale shauri lao la msingi litakaposikilizwa.

Awali, Mahakamani hapo Wakili Mkuu wa Serikali, Mhe. Gabriel Malata ambaye anaiwakilisha Serikali katika shauri hilo alisema kuwa wameyasikia maombi yaliyoletwa na waleta maombi mbele ya Mahakama na kuongeza kuwa wako tayari kupitia hoja zilizomo katika maombi hayo na kuzijibu ili kutimiza ibara ya 13(6)(a) inayotaka uwepo wa usawa mbele ya sheria.

Aliongeza kuwa kwa kutambua uwepo wa Mahakama, kifungu cha 68 na 95 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai inasema chombo cha utoaji haki nchini kitakuwa Mahakama hivyo wanaiachia Mahakama ili iweze kutoa uamuzi kulingana na maombi yaliyopo mbele yake.

Kwa upande wao Mawakili Peter Kibatala na Jeremiah Mtobesya walioiwakilisha CHADEMA waliwasilisha Mahakamani hapo hoja nane za kupinga kukubaliwa kwa zuio hilo Mahakamani hapo ambazo zilijikita kwenye madai ya kasoro zilizopo kwenye hati ya kiapo cha waombaji.

Kibatala alidai kuwa kiapo kilichowasilishwa Mahakamani hapo kina dosari ya kutotanabaishwa kwa dini za waapaji (Mdee na wenzake), hatua inayoleta wasiwasi kama walalamikaji waliapa kwa kutambua ukweli kuwa mlalamikaji anapoapa anapaswa kutaja na dini yake ili Mahakama iweze kujua aliapa kwa kutumia njia gani.

"Viapo vyao vilivyowasilishwa havitaji dini zao, hatua inayopelekea ikitokea wanataka kuapa Mahakama itashindwa kujua watatumia vitabu gani", alisema Wakili Kibatala.

Akiwasilisha hoja nyingine, Wakili Kibatala alidai Mahakamani hapo kuwa waombaji wameomba waendelee na nyadhifa zao bila kueleza hoja hizo zinakwenda kwa nani kwa kuwa hazisemi kama zimeelekezwa kwa Spika wa Bunge, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) au kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ana maslahi katika shauri hilo.

Kibatala alisema kuwa waombaji waliomba nafuu ya kuendelea kuwa wanachama wa CHADEMA bila kubainisha nafuu hiyo waipate kwa nani, hivyo Kibatala aliiomba Mahakama hiyo kutupilia mbali ombi hilo kwa kuwa kiapo hicho hakijakidhi sharti la zuio linalotaka waleta maombi kueleza moja kwa moja juu ya hatari gani inayoweza kutokea iwapo Wabunge hao wataondolewa bungeni.

Mawakili wa upande wa waleta maombi wakiongozwa na Wakili Aliko waliiomba Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kutoa amri ya zuio hilo kwa kuwa wajibu maombi hawana hoja za msingi za kuzuia Mahakama kutotoa zuio hilo kwa kuwa haijaweka wazi sheria inayotaka waapaji wataje dini zao wakati wanapokula kiapo.

Baada ya Mhe. Jaji John Mgeta kusikiliza pande zote mbili alisema kuwa Mahakama hiyo inazuia Wabunge hao kuondolewa kwenye nyadhifa zao hadi shauri la msingi lililofunguliwa na Wabunge hao litakaposikilizwa mnamo Juni 13 mwaka 2022.

> ***Mahakama inazuia Wabunge hao kuondolewa kwenye nyadhifa zao hadi shauri la msingi lililofunguliwa na Wabunge hao litakaposikilizwa***
>
> Mhe. John Mgeta
>
> **Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania**



*Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Prof. Sifuni Mchome (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dodoma.*

# BARAZA LAKAMILISHA MKATABA WA KWANZA

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliunda Mkataba wa Kwanza wa Baraza la Wafanyakazi wa Miaka Mitatu (Kuanzia Mwaka wa Fedha 2019/20 hadi 2021/22) ikiwa ni kwa ajili ya Utekelezaji wa sera ya kuwashirikisha wafanyakazi katika mchakato wa maamuzi kwa lengo la kujenga uongozi wa pamoja katika utekelezaji wa kazi na majukumu ya umma mahali pa kazi.

Ushirikishwaji huo wa wafanyakazi mahali pa kazi umeainishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 (The Public Service Act, No. 8 of 2002) pamoja na Kanuni zake za mwaka 2003 (Kanuni ya 108), Sheria ya majadiliano ya pamoja ya mwaka 2003 (The Public Service Negotiation Machinery Act, 2003 (no 19 of 2003), Kifungu cha 30 (3) na Sheria ya Ajira na mahusiano kazini Na. 6 ya Mwaka 2004 Kifungu cha 73 (1), (2).

Kwa mujibu wa Mkataba huo Ofisi ilihitajika kufanya Mikutano miwili katika kila Mwaka wa Fedha ikiwa Mkutano wa kwanza ni kwa ajili ya kupitia Makadirio ya Bajeti iliyopendekezwa kulingana na ukomo wa Bajeti na Mkutano wa pili ni kwa ajili ya kupitia utekelezaji wa bajeti iliyomaliza muda wake.

Matunda ya kuwa na Baraza la Wafanyakazi mahala pa kazi katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yameanza kuonekana. Matunda hayo ni pamoja na kuwashirikisha wafanyakazi katika maamuzi mbalimbali kama vile kuupitia kwa pamoja Mpango Mkakati wa OWMS wa Miaka Mitano (2020/2025), Wafanyakazi kushirikishwa juu ya mambo mbalimbali ikiwemo kuwasilisha changamoto mbalimbali na kuzitafutia ufumbuzi.

Aidha, baadhi ya utekelezaji wa Maazimio ya Baraza ilikuwa kuandaliwa kwa Mpango wa Mafunzo ulioanza utekelezaji wake Mwaka wa Fedha 2020/21, kuanzisha mfuko wa hiari wa kusaidiana, kukamilisha Mwongozo wa UKIMWI/VVU na magonjwa sugu yasiyoambukizwa.

Kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19, Baraza liliazimia elimu juu ya ugonjwa huu itolewe kwa watumishi wote na tahadhari ichukuliwe.

Mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa wajumbe yenye lengo la kutoa elimu na kuwajengea uwezo wajumbe kwenye masuala mbalimbali kwa kuzingatia majukumu na wajibu walionao kwa manufaa ya Ofisi katika kufikia malengo yake. Aidha, mafunzo hayo yameleta tija katika kuongeza ufanisi wa uendeshaji wa vikao vya Baraza la Wafanyakazi kwa Wajumbe.



*Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa katika Kikao cha Pili cha Baraza hilo kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 kilichofanyika jijini Dodoma.*

# WATUMISHI WASHIRIKISHWE UONGOZI WA PAMOJA

Mabaraza ya Wafanyakazi ndilo jukwaa la kisheria la majadiliano ya pamoja kati ya Viongozi na Watumishi katika Utumishi wa Umma kuhusu wajibu na maslahi ya Watumishi. Uundwaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi, ni Agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la mwaka 1970 na ni utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 Kifungu 73(1-3), kinachoelekeza juu ya kutekeleza Sera ya kuwashirikisha Wafanyakazi katika uongozi wa pamoja.

Mabaraza haya hufanyika mara mbili kwa mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma Na. 19 ya mwaka 2003 ambapo baraza la kwanza linakuwa na jukumu la kujadili na kupitisha bajeti, wakati baraza la pili ni kwa ajili ya kujadili utekelezaji wake.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali(OWMS) kama zilivyo Taasisi nyingine za Serikali iliamua kuunda na kuanzisha Baraza la Wafanyakazi litakalokuwa kiungo muhimu cha kushughulikia masuala mbalimbali kwa lengo la kukuza uwazi na ushirikishwaji katika maamuzi mbalimbali ili mfanyakazi anapotekeleza majukumu yake awe akifahamu Mpango Mkakati wa Miaka mitano ijayo ya OWMS na nini anatakiwa kufanya kulingana na Mpango Kazi wa Mwaka wa Fedha husika ili aweze kuisaidia Taasisi kufikia malengo yake kwa wakati.

Kupitia mabaraza haya, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imekuwa ikiwashirikisha watumishi wake katika masuala mbalimbali ikiwemo kupitia na kujadili bajeti ya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha husika, sambamba na kujadili utekelezaji wa Bajeti hiyo jambo ambalo ni sharti la msingi kutekelezwa, hatua ambayo imesaidia kila Mtumishi wa OWMS

kufahamu nini kimepangwa kutekelezwa kwa mwaka ujao wa fedha na huduma ya kiwango gani inapaswa kutolewa kwa mteja ili kufikia malengo ya Ofisi.

Ushirikishwaji wa mabaraza hayo katika mchakato wa bajeti sio jambo la hiari bali ni matakwa ya kisheria hivyo wasiounda mabaraza na wale wasioitisha vikao vya mabaraza kujadili bajeti za taasisi zao wanavunja sheria na hili ni jambo lisilovumilika.

Kwa kufanya hivi imewasaidia watumishi wa OWMS kujua bajeti iliyotengwa kwa ajili ya shughuli za ofisi ndani ya Taasisi ambapo imewawezesha watumishi wa OWMS kwa ujumla kufanya kazi kwa kuzingatia malengo na rasilimali zilizokadiriwa kutumika ndani ya muda husika hatua ambayo imesaidia kurahisha utekelezaji wa bajeti ya OWMS kwa kuwa imewasaidia watumishi hao kuendesha shughuli zao kulingana na mpango kazi wa Ofisi na hivyo kuwa rahisi kufikia malengo waliyojiwekea kila mwaka kwa urahisi zaidi.

Aidha, Ofisi imetumia mabaraza haya kupitia na kupisha miongozo mbalimbali ikiwemo Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, kupitia Mpango Mkakati, Mwongozo wa ulipaji wa ndani, kuandaa Kanuni za uendeshaji wa Mfuko wa kufarijiana pamoja kuwasilisha changamoto mbalimbali zinazowakabili watumishiiliziwezekutafutiwa ufumbuzi na Menejimenti kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali.

Mabaraza haya yamekuwa jukwaa muhimu sana mahala pa kazi ndani ya OWMS kwani yamefanikiwa kuepusha migogoro ambayo ingeweza kujitokeza baina ya wafanyakazi kwa wafanyakazi na Menejimenti kwa kuzingatia ukweli kuwa yamekuwa kiunganishi muhimu kati ya Menejimenti na Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kuleta ufumbuzi wa masuala ndani na nje ya ofisi.

Ikumbukwe kuwa Serikali inazingatia sana suala la Taasisi zake kuwa na mabaraza ya wafanyakazi ndio maana yalianzishwa kisheria kwa madhumuni ya kuishauri Serikali katika ngazi za idara na Vitengo, Taasisi na Wizara kuhusu usimamizi wa kazi na rasilimali watu, utekelezaji wa majukumu, kulinda haki na wajibu wa waajiri na wafanyakazi, kutoa ushauri kuhusu kujenga hali bora za kazi, maslahi ya wafanyakazi na kusimamia haki na ustawi mahala pa kazi.

Kufuatia hatua hiyo ndio maana hatuwezi kuzungumzia utawala bora mahala pa kazi bila ya kuwa na ushirikishwaji wa wafanyakazi. Ushirikishwaji wa wafanyakazi, unawezekana tu pale ambapo yapo mabaraza ya kazi yanayofanya kazi kwa kuwa Mabaraza haya ni fursa kwa wafanyakazi kuwakilishwa na kujenga madaraja kati ya menejimenti na wafanyakazi.

Aidha, Mabaraza haya hujenga mazingira ya kuwezesha madai ya wafanyakazi kufika katika menejimenti, na uamuzi kufanywa na mrejesho wa menejimenti kuwafikia wafanyakazi kupitia wajumbe wa baraza hatua inayoongeza uwajibikaji miongoni mwao yaani Menejimenti na Watumishi ndani ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Kupitia vikao vya mabaraza haya watumishi hupata fursa ya kuonyeshwa wazi utendaji wa kila idara hususani kwa mtu mmoja mmoja kulingana na vipimo vya utendaji wake, hali inayowasaidia wafanyakazi wa OWMS kufuata utaratibu unaoelekezwa pale bajeti hiyo inapoanza kutekelezwa na hivyo kusaidia pamoja na mambo mengine ili kuepuka hoja za ukaguzi zinazoweza kujitokeza.

Kupitia mabaraza haya pia watumishi wa Ofisi waliweza kuibua changamoto ambazo zilijadiliwa kwa pamoja na kutolewa mapendekezo ya namna bora ya kuzitatua.

Ni rai yangu kuwa mwisho wa baraza hili, uwe ndio mwanzo wa mabaraza mengine yatakayokuwa chachu ya kuongeza morali kwa watumishi kwa kuboresha mazingira ya watumishi na kuendelea kuwa daraja madhubuti kati ya Menejimenti na watumishi katika kutatua changamoto zinazowakabili kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma ili kuhakikisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inafikia malengo yake kwa wakati.




*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa kwenye picha ya pamoja walipotembelea Hifadhi ya Taifa ya Tarangire iliyopo mkoani Manyara*

# WATUMISHI WATEMBELEA HIFADHI YA TAIFA TARANGIRE

Wakili Mkuu wa Serikali, Mhe. Gabriel Malata, amewasihi wananchi kujenga tabia ya kutembelea vivutio vya utalii nchini ikiwemo Hifadhi za Taifa na mambo ya kale kwa lengo la kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassani katika kukuza sekta ya utalii nchini.

Mhe. Malata alitoa wito huo wakati alipowaongoza watumishi wa Ofisi ya Wakili

Mkuu wa Serikali kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Tarangire kwa lengo la kujionea vivutio mbalimbali vinavyopatikana ndani ya hifadhi hiyo.


Akiwa kwenye hifadhi hiyo, Mhe. Malata alisema kuwa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan anafanya kazi kubwa ya kujenga uchumi wetu kupitia sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya utalii nchini ndio maana ameamua kushiriki moja kwa moja katika filamu ya *The Royal Tour Tanzania* ambayo ameitumia kutangaza vivutio mbalimbali vinavyopatikana nchini kwa ulimwengu wote.

"Mhe Rais anafanya kazi kubwa sana hasa kwenye kutangaza vivutio vya utalii nchini hivyo hatuna budi kumpongeza na kumuunga mkono kwa kutembelea vivutio vyetu vya ndani", alisema Mhe. Malata.

Aliongeza kuwa kufanya utalii siyo lazima mtu aende nchi za nje, hata safari za ndani ya nchi au ndani ya eneo lako unaloishi zina maana kubwa, hasa kama zitafanywa kwa lengo la kujifunza. Kwa kuwa mtu anapofunga safari ya kutembelea vivutio na maajabu ni njia nzuri ya kuona fursa zilizopo kwenye eneo fulani unazoweza kuzifanyia kazi na ukajipatia kipato ikiwa ni pamoja na kujiburudisha.

Akizungumzia faida za utalii nchini, Mhe. Malata alisema kuwa pamoja na mambo mengine utalii una faida kubwa kwani shughuli zinazofanywa wakati wa utalii hufaidisha pande zote mbili yaani mtalii unapotembelea vivutio hivyo nchini kwako, utaburudika sana na kuelimika ikiwa ni pamoja na kuchangia pato la taifa ambapo fedha zinazopatikana zinatumika kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kwa manufaa ya Taifa.

Aliongeza kuwa Tanzania kama nchi tunayo bahati ya kuwa na maeneo muhimu kwa utalii kama vile hifadhi za taifa kwa mfano kama hapa Tarangire; mapori ya tengefu ya akiba; fukwe za bahari; maeneo ya kihistoria kama vile Kaole kule Bagamoyo; milima; maziwa; na vingine vingi hivyo, unaposafiri unajifunza mambo mbalimbali ambayo isingekuwa rahisi kujifunza ukiwa nyumbani.



*Tembo akivuka barabara ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire kama alivyokutwa na mpiga picha wetu.*



Kuro

Alisisitiza kuwa wananchi wanapotembelea maeneo kama haya ya vivutio wanapata fursa mbalimbali za kujifunza jiografia, utamaduni au hata mtindo wa maisha wa watu wa maeneo wanayotembelea ikiwa ni pamoja na kuchangia uchumi wa eneo husika kwa kununua bidhaa mbalimbali zinazopatikana kwenye maeneo hayo.



Kuhusu namna nchi inavyoweza kuongeza kipato Mhe. Malata alisema kuwa kutembelea maeneo mbalimbali ni shule nzuri ya kuongeza maarifa. Ifahamike wazi kuwa, nchi zinazowahudumia watalii hujipatia fedha nyingi za kigeni kwa kuwa nchi yoyote huhitaji fedha za kigeni zitakazosaidia kurahisisha utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kama mradi wa Bwawa kubwa la umeme, reli ya kisasa (SGR) iliyopo nchini Tanzania ambayo inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita.

Aidha, alieleza kuwa faida nyingine ya kutembelea vivutio vya utalii ni pamoja na kupumzika; kufurahia mazingira lakini kupitia utalii watu wanaweza kugundua fursa mbalimbali zikiwemo za uwekezaji zinazopatikana katika maeneo ya utalii na hivyo kusaidia kuwekeza na hatimaye kuongeza pato la taifa ikiwemo kupunguza tatizo la ajira nchini.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali waliotembelea hifadhi hiyo waliishukuru Ofisi kwa kuandaa ziara hiyo kwa kuwa imewasaidia kujionea kwa macho vivutio mbalimbali vinavyopatikana nchini hali iliyosaidia kuwaongezea morali ya kutekeleza majukumu yao mara tu watakaporejea katika vituo vyao vya kazi.

Akizungumza kwa niaba ya watumishi hao, Mkurugenzi Msaidizi wa Usimamizi wa Mashauri, Bw. Abubakar Mrisha alisema kuwa ziara hii ni muhimu kwa kuwa imesaidia kuiweka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali karibu na wadau lakini sisi wenyewe kama watumishi imetusaidia kuwa pamoja hali ambayo imeongeza mshikamano miongoni mwetu.

Aliongeza kuwa ziara hii itasaidia kuongeza morali miongoni mwa watumishi hao hali itakayosaidia kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri kwa niaba ya Serikali.

Bw. Mrisha alisema kuwa ziara hii itawarahisishia kazi zao hasa pale watakapotakiwa kushughulikia migogoro kati ya Hifadhi na wananchi kwa kuwa sasa watumishi hao hasa Mawakili wamepata wasaa wa kujionea maeneo mbalimbali ikiwemo mipaka ya hifadhi hiyo ikiwa ni pamoja na kuwa mabalozi wazuri katika kutangaza vivutio mbalimbali vinavyopatikana nchini.


Kabla ya ziara hiyo watumishi walipata fursa ya kushiriki kikao ya siku nne yaliyokuwa na lengo la kuwajengea uwezo kuhusu namna bora ya kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi katika nyanja mbalimbali za kisheria.




Tumbili



*Baadhi ya Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa katika picha ya pamoja walipotembelea Hifadhi ya Taifa ya Tarangire - Manyara.*




Pundamilia



Twiga



*Wakili Mkuu wa Serikali, Mhe. Gabriel Malata (katikati waliosimama) akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili wa Serikali walipotembelea Hifadhi ya Taifa ya Tarangire - Manyara.*



Swala Pala



Nguchiro





*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa katika picha ya pamoja walipotembelea Hifadhi ya Taifa ya Tarangire - Manyara.*

JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**
**10 Barabara ya Kivukoni**
**S. L. P 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Nukushi: www.osg.go.tz**
**Barua pepe: info@osg.go.tz**

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

| | |
|---|---|
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1902<br>41218 DODOMA<br>Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)<br>Barua pepe: dodoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 130<br>31101 MUSOMA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mara@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1280<br>63114 MTWARA<br>Maadili House<br>Barua pepe: mtwara@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 394<br>33101 MWANZA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mwanza@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 595<br>51108 IRINGA<br>Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa<br>Barua pepe: iringa@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 106<br>35102 BUKOBA<br>Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mhakiki Mali<br>Barua pepe: kagera@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 564<br>57101 SONGEA<br>Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 43<br>37101 SHINYANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 60<br>21101 TANGA<br>Jengo la Mkonge<br>Barua pepe: tanga@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 119<br>45112 TABORA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: tabora@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 202<br>25101 MOSHI<br>Jengo la TRA Moshi<br>Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 321<br>55103 SUMBAWANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: rukwa@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 66<br>23101 ARUSHA<br>Jengo la AICC, Arusha<br>Barua pepe: arusha@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 710<br>53107 MBEYA<br>Jengo la Madini<br>Barua pepe: mbeya@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 172<br>47101 KIGOMA, Jengo la NHC, Ghorofa ya Pili,<br>Kiwanja Na. 148 & 149, Mtaa wa Lumumba.<br>Barua pepe: kigoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>Jengo la NSSF, Ghorofa la Pili<br>MOROGORO, Barabara ya zamani DSM<br>Barua pepe: morogoro@osg.go.tz |